

UWATA SHULE YA AWALI NA MSINGI MCHUO WA KIINGEREZA

Tel: +255-25-2510051

Mobile: +255-763-674878

+255-754-432411

Fax: +255-25-2510341



S.L.P. 3574,
MBEYA

Email: uwataprimarys@yahoo.com

FOMU YA USAILI (INTERVIEW FORM) YA KUJIUNGA NA SHULE YA AWALI

Gharama ya fomu ni 25,000/=

NAMBA YA FOMU: _____

A: MAELEKEZO YA AWALI

1. Fomu hii ijazwe kwa herufi kubwa.
2. Fomu hii ijazwe na mzazi/mlezi wa mwanafunzi anayetaka kujiunga na shule ya awali na msingi.

Picha ya Mzazi

Picha ya Mwanafunzi

B : HABARI ZA MWANAFUNZI

1. Jina kamili la mwanafunzi
2. Umri wa mwanafunzi Jinsia yake MV/MS:
3. Mahali anapoishi WILAYA: MKOA:

C: HABARI ZA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la Mzazi/Mlezi
2. Kazi anayofanya
3. Mahali anapoishi
4. Anuani ya Mzazi/Mlezi
5. Namba ya simu: Mkononi Kazini :

Nyumbani :

D: MAELEKEZO MUHIMU

- Usaili utafanyika siku ya jumamosi tarehe 10/12/2016 kuanzia saa 2:00 asubuhi na mwanafunzi atakayechelewa zaidi ya nusu saa hataruhusiwa kuingia.
- Siku ya usahili mzazi/mlezi unapaswa kuleta kivuli cha cheti cha kuzaliwa cha mtoto na kiambatanishwe na fomu hii ikiwa imejazwa kikamilifu na kubandikwa picha ya mzazi/mlezi na mwanafunzi.
- Mwanafunzi anayestahili kuanza shule ya awali awe angalau na umri usiopungua miaka mitatu na nusu ($3\frac{1}{2}$).
- Mwanafunzi anayeomba nafasi ya awali endapo atachaguliwa kujiunga na shule yetu hatapewa nafasi ya bwani kulingana na umri wake, hivyo wanafunzi wote wa awali watatokea nyumbani kwa miguu au kwa magari ya shule.
- Mwanafunzi anayeomba nafasi ya shule ya awali (chekechea) atafanya usaili wa mdomo (Oral Interview), kwa kuulizwa maswali machache ya kijamii, na mtoto atakayeweza kujieleza vizuri na kupata alama angalau 70% atakuwa amefaulu kujiunga na shule yetu.
- Kituo cha usaili ni kimoja tu, yaani uwata shule ya msingi. Na matokeo yatatolewa siku tatu baada ya mtihani yaani Jumatatu tarehe 12/12/2016.
- Baada ya kufaulu na kufahamishwa kuwa amepata nafasi Mzazi/Mlezi utachukua fomu ya maelekezo (Joining instruction) kwa Tsh.15,000/=), fomu zitatolewa kuanzia Jumatatu tarehe 12/12/2016 mpaka ijumaa tarehe 16/12/2016, endapo mzazi/mlezi utashindwa kuchukua fomu kwa muda huo basi nafasi hiyo atapewa mwingine..

E: SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE KWA MWANAFUNZI WA KUTWA NA BWANI

1. Mtoto haruhusiwi kusuka nywele
2. Mtoto atapokelewa hapa shuleni iwapo hana magonjwa ya kuambukiza.
3. Huruhusiwi kumwachia mtoto kiasi chochote cha fedha mkononi mwake au kumletea chakula mwanafunzi wa bwani
4. Mwanafunzi anapaswa kuongea kiingereza awapo shuleni isipokuwa kwenye somo la Kiswahili.

5. Kila mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu watu wote.
6. Mwanafunzi anapaswa kuwahi shuleni kwa muda unaotakiwa.
7. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kuvuta sigara, kunywa pombe na kutumia madawa ya kulevya, kutukana matusi, kupigana na kujihusisha katika vitendo vya mapenzi na adhabu yakufukuzwa shule.
8. Mwanafunzi haruhusiwi kujihusisha na vitendo vya kishirikina kwa maneno au matendo. Pia kuvaa hirizi na kutumia madawa yasiyo thibitishwa na daktari.
9. Kila mwanafunzi ni lazima kuhudhuria vipindi vya ibada, neno la mungu na maombi bila kujali tofauti ya dini ya mwanafunzi husika kwani shule hii ni ya kikristo.
10. Mwanafunzi atokapo nje ya shule ni sharti avae sare za shule.
11. Ni marufuku mwanafunzi kuharibu mali za shule, mara ikibainika kufanya hivyo kwa makusudi mzazi/mlezi atatakiwa kulipa fidia kwa mali hizo.

MOTTO WA SHULE '**ELIMU NI UKOMBOZI**'

E. ABEL

MKUU WA SHULE